# ULINZI WA WATOTO KIPINDI CHA JANGA LA COVID-19

## Watoto na Malezi Mbadala

*Hatua za haraka za Kukabiliana*



Uandaaji wa dokezo hili la kiufundi umaratibiwa na Better Care Network, The Alliance for Child Protection in Humanitarian Action na UNICEF

Better Care Network

THE ALLIANCE FOR CHILD PROTECTION IN HUMANITARIAN ACTION

unicef for every child

## UTANGULIZI

Ushahidi kutoka kwenye milipuko ya magonjwa ambukizi iliyotokea huko nyuma inaonesha kuwa hatari za ulinzi wa mtoto zinaongezeka na hatari mpya hujitokeza kutokana na mlipuko wa ugonjwa pamoja na matokeo ya kijamii na kiuchumi katika kuzuia na hatua za kudhibiti. Baadhi ya watoto wanakuwa katika hatari kubwa zaidi katika mazingira kama haya hasa wale wanaoishi bila uangalizi wa wazazi au familia, walio katika hatari ya kutenganishwa na familia zao, walio katika mfumo wa malezi mbadala na wale waliotoka katika mfumo wa malezi mdadala hivi karibuni.

Kusudi la dokezo hili la kitalaamu ni kusaidia watendaji wa ulinzi wa watoto na maafisa wa serikali katika mwitikio wao wa hatua za haraka kukabiliana na changamoto za ulinzi wa watoto zinazowakabili wale ambao wako katika hatari ya kutenganishwa na familia zao au wako kwenye mfumo wa malezi mbadala katika kipindi hiki cha janga la COVID-19. Imeandaliwa na wafanyakazi wa kikosi cha wataalam maalumkutoka taasisi mbalimbali walio bobea katika ulinzi na na malezi ya watoto na linajengea kwenye dokezo la kitaalam: ***Ulinzi wa watoto wakati wa Janga la Virusi vya Corona*** lililoandaliwa na ***The Alliance for Child Protection in Humanitarian Action*** na lina msingi wa viwango vya kimataifa na utendaji katika malezi na ulinzi wa watoto[1].


*Picha Na: Argenziano, Italy, Unsplash*

[1] Dokezo hili la kitaalam limeandaliwa kwa viwango vya Kimataifa vinavyotumika, Pamoja na Convention on the Rights of the Child, the Convention on the Rights of Persons with Disabilities, the Guidelines for the Alternative Care of Children and the 2019 Child Protection Minimum Standards, Hasa : Kiwango cha 13: Watoto wasioambatana na wazazi/walezi na watoto waliotengwa; Kiwango cha 16: Kuimarisha familia na mazingira ya utunzaji wa watoto; Kiwango cha 18: Usimamizi wa kesi (Case management ); Kiwango cha 19: Malezi mbadala.

Nyumbani
Utangulizi
Athari ya covid-19 kwa watoto waliokatika hatari ya kutenganishwa au walio katika malezi mbadara
Njia za programu
Kuwaweka watoto salama katika malezi ya familia
Ulinzi wa watoto katika malezi mbadala
Ulinzi wa watoto katika mazingira ya mtaani
Kusaidia vijana wasio katika malezi na wanaoishi kwa kujitegemea
Taarifa zaidi

## ATHARI YA COVID-19 KWA WATOTO WALIOKATIKA HATARI YA KUTENGANISHWA AU WALIO KATIKA MALEZI MBADARA

Machafuko yanayosababishwa na COVID-19 pamoja na hatua zinazochukuliwa kuzuia ugonjwa huo huathiri watoto, familia na mazingira kwa ujumla. Hatua za dharura za kukabiliana na ugonjwa huu hupelekea kufungwa kwa baadhi ya huduma za kijamii na kusababisha utegemezi kwa kiasi kikubwa hasa kwa wale ambao ni tegemezi tayari. Familia zenye mazingira yanayoainishwa na hali ya umaskini au rasilimali duni zitalemewa zaidi na mikakati inayochukuliwa kukabiliana na ugonjwa huu kama vile zuio la kutembea na matumizi ya usafiri wa umma na hivyo kusababisha watu kukosa ajira au kuwa na kipato duni, kufungwa kwa shule, upatikanaji duni wa huduma na msaada wa kijamii, janga la njaa na hali ya kutengwa na jamii. Mazingira ya nyumbani yenye msongo wa mawazo yanaongeza uwezekano wa unyanyasaji wa kijinsia majumbani, pamoja na migogoro ya kifamilia, unyanyasaji na machafuko baina ya watu.



*Picha Na: Araujo, Unsplash*

**Athari za janga kwa watoto, familia, na jamii zinatofautiana kulingana na muktadha na hatua na kiwango cha janga hilo. Vile vile, kuna uwezo tofauti wa mifumo - mifumo ya serikali kwa jumla haswa mifumo ya ulinzi wa na usalama kwa watoto, ili kukabiliana na athari ya janga kwa watoto na familia.**

Inategemewa kuwa idadi ya watoto walio katika hatari ya kutenganishwa na familia zao pamoja na wale wanaohitaji malezi mbadala itaongezeka – Kwa pamoja kipindi cha janga hili ambapo hatua zinazochukuliwa kukabiliana na janga hili zinaweza kupelekea watoto kutenganishwa na familia zao na kutokana na matokeo ya muda mrefu ya athari ya kijamii na kiuchumi kutokana na janga la COVID-19 kutakuwa na changamoto kwa famlia kuwa na uwezo wa kulea Watoto.

Katika hali nyingi, wazazi na walezi wengine wa msingi wataweza kutegemea wanafamilia wengine na ndugu kusaidiamalezi ya watoto wao; Ijapokuwa, kwa baadhi ya kesi utaratibu wa malezi mbadala utahitajika. Jitihada za kuongeza nguvu mahususi katika kujenga uwezo wa familia kwenye malezi malezi ya Watoto katika makao bila ulazima wowote.

**Jitihada za kuongeza nguvu mahususi za uwezo wa utunzaji wa watoto katika familia na mifumo ya ulinzi wa jamii ni muhimu ili kuongeza utulivu wa kifamilia na kuzuia kushughulikia utunzaji wa makazi ya watoto usio lazima.**

### Watoto walio tayari Katika mfumo wa malezi mbadala wanakabiliwa na changamoto zifuatazo:

- **Walezi wa kambo,** haswa babu/bibi na / au wazee, wanaweza kuachana na majukumu hayo kwa muda kutokana na hali zao za kiafya kuwa matatani na athari za kifedha kutokana na janga la COVID-19 kwenye huduma za malezi ya kambo pia kusababisha kutelekezwa kwa watoto katika aina hii ya malezi.
- Hatari kwa watoto katika mazingira ya vituo vya malezi ni kufungwa ghafla kwa makao na watoto kurudishwa kwenye familia na katika jamii zao bila maandalizi ya kutosha. Hatari zinaweza pia kusababishwa kwa watoto kubaki katika makao ambapo mazingira ya watu wengi yanaweza kurahisisha kuenea kwa ugonjwa na kuwaathiri watoto wanaoishi humo huku wakiwa katika hatari kubwa ya unyanyasaji, kupuuzwa na unyonyaji. Hii ni hatari kubwa hasa kwa watoto wenye ulemavu, ambao wana uwezekano mkubwa wa kuwa katika makao na katika hali zingine (Kutokana na hali maalum ya awali au ulemavu, pamoja na kinga pungufu) wanaweza kuwa katika hatari kubwa ya kuambukizwa COVID-19 na kuathirika zaidi.
- Watoto wanaoishi katika mazingira ya kujitegemea wanaweza kuwa katika hatari kubwa ya kutengwa na kutengana na kundi rika lao, na pia kukosa pesa na aina nyingine za msaada kwa mahitaji yao ya kila siku.
- Baadhi ya watoto wanaoishi kwenye mfumo wa malezi mbadala na hawana furaha na makazi hayo, watashindwa kuvumilia hali ya kuwekwa kizuizini kwa nguvu. Wengine ambao wanakuwa wametoka katika mfumo wa malezi mbadala wanaweza kukumbana na hali ya kutengwa na jamii na kujikuta wakikosa msaada wa kifedha na misaada mingine muhimu katika kipindi hiki kigumu.

Kwa watoto waishio mitaani, wakimbizi, na wahamiaji, upatikanaji wa msaada na huduma utakuwa mgumu sana kutokana na sheria za kufungwa kwa miji pamoja na huduma za kijamii na wanaweza hata kukamatwa na kuwekwa kizuizini. Watoto wakimbizi na wahamiaji pia wanaweza kuzuiwa kupata huduma muhimu kwa sababu ya vizuizi vya kisheria, nyaraka, lugha au vikwazo vya kiusalama.

## NJIA ZA PROGRAMU

Kushirikisha na ushiriki wa wadau wote ni msingi wa kudumisha mwendelezo wa huduma kwa watoto. Sekta ya malezi inajumuisha safu kubwa ya wadau mbalimbali, ikiwa ni pamoja na watoto, vijana, familia, serikali, asasi za kiraia, wafadhili, na wengine. **Tafadhali bofya hapa kusoma vidokezo muhimu juu ya:**

- Kushirikisha watoto, familia, walezi na jamii, pamoja na viongozi wa imani/dini.
- Kufanya kazi katika Sekta zote na serikali.
- Kushirikiana na wafadhili



*Picha Na: Save the Children*

**MAREJELEO**

[2] Preventive and Responsive Support to Children, Families and Alternative Care Providers During COVID-19 (Changing the Way We Care)

[3] What Parents Should Know (UNICEF)

Positive Parenting (End Violence)

Protection of Children During Infectious Disease Outbreaks (The Alliance)

[4] COVID-19 and the Disability Movement (IDA)

[5] Mental Health Considerations During COVID-19 (WHO)

Addressing Mental Health and Psychosocial Aspects of COVID-19 (IASC)

Psychological Coping During a Disease Outbreak (PS Centre - IFRCRC)

## KUWAWEKA WATOTO SALAMA KATIKA MALEZI YA FAMILIA

Serikali na asasi za kiraia zinapaswa kupanga msaada ulioimarika kwa familia na jamii ili kuweka kipaumbele usalama wa watoto katika mazingira ya familia. Familia zitafanya maamuzi juu ya malezi, wakati watendaji watazisaidia familia kutambua msaada unaohitajika ili kuhakikisha wanaweza kuishi kwa usalama[2]. Kuziwezesha familia kukabiliana kwa usalama, kutahitaji kupunguza changamoto kama vile kukosekana kwa chakula na uchumi mbovu na kuongeza uwezo uelewa kwenye malezi bora[3]. Msaada kama huo utapunguza hatari ya mazoea mabaya kama vile ajira kwa watoto, ndoa za utotoni na usafirishaji haramu wa watoto.

**Nini kifanyike kuzuia watoto kutenganishwa na familia zao na kuwalinda watoto wakiwa katika malezi/uangalizi wa familia:**

- Kutoa Elimu kwa familia, walezi, na watoto juu ya namna ya kuzuia kuenea kwa COVID-19, ikiwa ni pamoja na mazingira ambayo kuna uhaba wa maji/sabuni, kuhakikisha rasilimali kama vile vifaa vya usafi vinapatikana, na kuhakikisha kuwa maarifa na rasilimali zinapatikana kwa watoto na au wazazi wenye ulemavu4[4].
- Kusambaza ujumbe unaojumuisha walemavu juu ya kujitunza, afya ya akili na msaada wa kisaikolojia[5], nidhamu chanya[6], tabia za watoto, na shughuli za nyumbani[7]. Kuwa makini na uhakikishe kuwa ujumbe unawafikia pia watu wenye ulemavu.
- Kwa kutambua na kuzingatia hatari za kiafya kwa wazee, hakikisha wale wanaotunza watoto wanapewa kipaumbele cha msaada na rasilimali[8].

[6] Parenting during COVID-19

[7] *Shujaa Wangu ni Wewe*

[8] COVID-19 Fact Sheet for Grandfamilies and Multigenerational Families (GU)

MHPSS During Disease Outbreak – Elderly (PS Centre - IFRCRC)

- Himiza na saidia familia kuchagua mtu atakaewalea watoto ikiwa mzazi au mlezi ataugua au atalazimika kuuguza mgonjwa aliye katika familia na uwahimize wanafamilia na jamaa kutoa msaada kutoka mbali kwa kutumia teknolojia inayopatikana[9].

- Ondoa vizuizi vya kupata manufaa kwa kuondoa vikwazo vinavyohusiana na upattikanaji fedha na kukuza upatikanaji wa fedha nje ya mahali pa makazi[10].

- Wajulishe familia, waalimu, watumishi wa afya na wafanyakazi wengine wa kazi za jamii juu ya namna ya kuwatambua na kuwaokoa watoto walio na mahitaji makubwa ya ulinzi na wale walio kwenye hatari kubwa ya kutenganishwa na familia zao pamoja na wale wenye ulemavu, kwa sababu ya kuwepo kwa kifo au mgonjwa katika familia zao[11].



*Picha Na: Save the Children*

- Kwa watoto ambao tayari wanajulikana kuwa katika hatari ya kutenganishwa na familia zao kabla ya janga kutokea, wafanyakazi wa huduma za kijamii wanapaswa kutoa msaada endelevu na ufuatiliaji kwa njia ya simu ya kawaida au anwani nyingine yoyote.

- Shirikisha viongozi wa jamii, pamoja na viongozi wa imani, kupambana na unyanyapaaji watoto na habari za uvumi juu ya COVID-19. Kwa wale ambao ni wagonjwa, waliowekwa wazi au wamepona ugonjwa huu, wasaidie kusambaza taarifa za msingi na ukweli juu ya dalili, namna ya ueneaji na namna ya kupata ahueni ikiwa umeugua ugonjwa huu (kwa kutumia redio, megafoni/mitandao ya kijamii n.k)[12].

- Watambue na uwajumuishe wahamiaji, wakimbizi, wasiofahamika mahali wanapotoka, watoto na familia zilizohama makazi ndani ya nchi kutokana na majanga, na wale wasio na taarifa katika hatua muhimu za kipaumbele kama vile upatikanaji wa huduma za afya kwaajili ya kujikinga, kupata matibabu na upimaji, mipango ya ulinzi kijamii, usambazaji rafiki wa taarifa kwa watoto, na njia mbalimbali za kutoa rufaa ikiwemo msaada kwa njia ya mtandaoni kama itawezekana[13].

**MAREJELEO**

[9] How to Talk to your Child about Coronavirus (UNICEF)
[10] Cash and Voucher Programming for Social Protection During COVID-19 (World Vision)
[11] Global Rapid Gender Analysis for COVID-19 (IRC)
[12] COVID-19 Stigma Guide
[13] Scaling Up COVID-19 Readiness and Response Operations including Camp and Camp-Like Settings (IASC
Quick Tips on COVID-19 and Migrant, Refugee and Internally Displaced Children (Children on the Move)

# ULINZI WA WATOTO KATIKA MALEZI MBADALA

Katika muktadha ambapo huduma za jamii zimepooza au kuzorota na kuna hitaji la hatua za kujitenga kwa watu katika jamii, ni muhimu kuweka kipaumbele katika msaada kwa watoa huduma wa malezi mbadala katika familia ( ndugu wa karibu na watu wa kuaminika) na kuhakikisha malezi ya watoto katika vituo vya kulelea watoto yanasimamiwa kwa umakini ndani ya kipindi hiki cha dharura.

Watoa huduma ya malezi mbadala na wafanyakazi wanaosimamia uwekwaji wa watoto katika huduma za malezi pia wanaathiriwa na hivyo mikakati mipya inahitaji kuwekwa haraka ili kukabiliana na tatizo hili. Kwa kuzingatia ukubwa na upeo wa dharura hii, kutakuwa na hitaji kubwa la utunzaji/malezi mbadala, haswa huduma ya mpito katika kipindi cha dharura, na watoa huduma wanapaswa kuwa na mipango mikakati ili kukidhi hitaji hilo.

**Vitu vinavyotakiwa kufanyika kuwalinda watoto katika mfumo wa malezi mbadala:**

- Mipango ya dharura inayojumuisha huduma katika malezi mbadala inapaswa kuandaliwa na mamlaka husika za ustawi wa watoto kwa kushirikiana na watoa huduma na viongozi wa jamii. Upangaji unapaswa kuzingatia uzito na muda wa dharura (hadi miezi 18). Katika maeneo ambapo mamlaka za ustawi wa watoto hazifanyi kazi, watendaji wa ulinzi wa watoto wanapaswa kufanya kazi na viongozi wa jamii na watoa huduma, ikiwa ni pamoja na wafanyakazi wa afya na wa elimu kuboresha mipango hii.

**Mipango hii inapaswa kujumuisha angalau:**

- Tamko wazi la sera ya kuweka kipaumbele katika njia mbadala za malezi kwa watoto katika familia zao badala ya makao lichapishwe na lisambazwe katika vituo vya huduma za afya, vituo vya polisi, mahakama, halmashauri za mitaa na miundo / mifumo ya kijamii ya ulinzi wa watoto.

- Huduma za malezi mbadala zinapaswa kufafanuliwa kama huduma 'muhimu' katika mfumo wa usimamizi wa dharura wa serikali.

- Taratibu mpya za utoaji wa huduma zinapaswa kujumuisha uchunguzi wa rufaa kupitia mitandao na simu, tathmini ya ulazima wa kuwaweka watoto katika malezi mbadala pamoja na idhini ya kuwaweka watoto katika malezi hayo na ufuatiliaji utakaofanywa na mamlaka ya ustawi wa watoto.

- Vizuizi au makatazo yanapaswa kuwekwa dhidi ya uwekwaji wa watoto katika makao kinyume na utaratibu katika kipindi hiki cha dharura. Watoa huduma wanapaswa kuzijulisha mamlaka husika punde tu mtoto anapopelekwa kwenye kituo pasipo kufuata taratibu rasmi wa utoaji huduma.

- Mamlaka husika zinapaswa kuweka Mwongozo wa Uendeshaji wa Kiwango kushughulikia mahitaji ya malezi ya muda kwa watoto waliotengana au wasioambatana na walezi wao, pamoja na mwongozo unaoeleweka juu ya hatua zitakazochukuliwa ikiwa mtoto amepatwa au anadalili za virusi na atahitaji kutengwa kwa kipindi fulani. Umakini mkubwa utahitajika katika kuzuia uwekaji usio lazima wa watoto katika vituo vya malezi katika kipindi hiki cha mapambano dhidi ya COVID-19 ikiwa ni pamoja na watoto wenye ulemavu[14].

- Mamlaka za ustawi wa watoto zinapaswa kutoa agizo la kusitisha ujenzi wa vituo vipya vya utunzaji wa watoto ambalo litawafikia watu wengi likiambatana na mwongozo na jumbe zinazosisitiza kuzingatiwa kwa njia zilizopo za utoaji huduma kwa watoto wapya katika vituo vilivyopo.

- Kila kituo cha utunzaji wa watoto kinapaswa kuainishwa kama sehemu moja ya makazi kwa madhumuni ya kutii kanuni / maagizo ya serikali juu ya kujitenga, na mwongozo unapaswa kusambazwa kwa watoa huduma wote juu ya maagizo ya kukaa mbalimbali, kujitenga na hatua za kuwekwa karantini ndani ya makazi hayo ya kutunzia watoto.

**REJEA**

[14] COVID-19 and the Disability Movement (IDA)

- Vituo vya utunzaji wa watoto havipaswi kufungwa horera na havipaswi kufanya kazi pasipo kutoa huduma bora na mipango ya msaada kwa kila mtoto.

- Serikali, kwa kushirikiana na watendaji wa usalama wa watoto, wanapaswa kutoa / kuhakikisha kuna upatikanaji wa mahitaji muhimu (chakula, vifaa vya usafi na dawa muhimu) na huduma muhimu (ikiwa ni pamoja na zile zinazohitajika sana kwa watoto wenye ulemavu) kwa watoa huduma wa malezi mbadala katika kipindi ambacho kutakuwa na vizuizi vya kusafiri na kufanya manunuzi au bidhaa kuwa adimu na ngumu kuzipata kwa njia za kawaida.

- Uhakiki na utambuzi wa wafanyakazi muhimu yanapaswa kufanyika ikiwa ni pamoja na watu wanaohusika na utambuzi wa kesi za maambukizi na rasilimali muhimu zinazohitajika katika kipindi hiki cha dharura huku kukiwa na wafanyakazi mbadala ikiwa wafanyakazi wengine watahitaji kukaa karantini. Pia lazima kuwe na mipango ya kupata fedha za kutosha kuziwezesha mamlaka za ulinzi wa watoto kuendesha shughuli za huduma katika kukabiliana na janga.

- Mwongozo wa Uendeshaji wa Kiwango (SOP) umnastahili kuandaliwa kwa kuzingatia uwekaji wa watoto katika familia kutoka kwenye akao ili walelewe na ndugu zao na hivyo kipaumbele kiwekwe katika kuwarejesha watoto katika familia zao. Taarifa za mahali mtoto aliporejeshwa lazima ziandikwe na mawasiliano ya huyo mtoto yawepo.

- Kuimarisha uwezo wa huduma za simu na vituo vya msaada vya watoto, ili watoto, familia na vituo vya utunzaji watoto viweze kuripoti kesi yoyote ya unyanyasaji au kupuuzwa.

*Picha Na: Nayeli Dalton, Unsplash*




**Vipaumbele vingine ni pamoja na;**

- Watoto wote, walezi na wafanyakazi wanapaswa kupokea mafunzo ya afya na usalama dhidi ya COVID-19, kwa kuzingatia ujumbe wa kupendeza watoto na njia za ufundishaji zinazowafaa hata watoto wenye ulemavu[15].

- Vifaa vya kutosha vya kinga binafsi (PPE) vinapaswa pia kutolewa kwa walezi wanaofanya kazi na watoto ambao wana magonjwa sugu au hali mbaya ya kiafya au ambao wapo katika mazingira hatarishi na pia katika hali ambayo kuna watu wengine ndani ya familia au katika kituo cha malezi wapo katika hatari ya kupata maambukizi.

- Familia au vituo vya malezi vinapaswa kupewa msaada wa ziada wa nyenzo, ikiwa ni pamoja na fedha, afya, na elimu, kwa kuzingatia gharama ya ziada ya kumtunza mtoto wakati wa janga hili.

**REJEA**

[15] Infection Prevention and Control guidance for Long-Term Care Facilities in the context of COVID-19 (WHO)

- Kuainisha na kupata vyanzo vya msaada zaidi kwa kushirikiana na mamlaka husika za afya ili kuhakikisha vituo vya malezi mbadala vina uwezo wa kukidhi mahitaji ya watoto wenye ulemavu, mahitaji maalum na au wale walio na maswala ya kimsingi ya afya ambao wanaweza kuathiriwa vibaya na COVID-19, ikiwa ni pamoja na kulazwa hospitali kama itahitajika[16].

- Watoa huduma ya malezi wa kuaminika wanapaswa kukagua kesi zote ili kujua kama kuna mtoto ambaye bado hajarudishwa kwenye familia yake. Azimio linapaswa kufanyika ikiwa bado inawezekana na ni salama kwa mtoto kurejeshwa katika familia yake na kama inaweza kuwa na faida kwa mtoto kurejeshwa katika familia. Mahitaji ya msaada kwa familia yanapaswa kutambuliwa na kupatikana ili kuwawezesha kumtunza mtoto ipasavyo.

- Huduma mkoba  kwa familia za walezi wa kuaminika waliopo na wapya zifanyike kutambua  kama watakuwa tayari kutunza mtoto mwingine, kwa msaada unaofaa ikiwa utahitajika. Familia za walezi wa kuaminika  wenye uzoefu wa malezi wanapaswa kutambuliwa kwaajili ya kuwaweka watoto ambao wanakabiliwa na hatari fulani, kama watoto wadogo na watoto wachanga, watoto na vijana ambao wamepitia ukatili, watoto wenye ulemavu wenye mahitaji maalumu ya matibabu au mahitaji mengine ya utunzaji, wahamiaji na watoto wakimbizi ambao hawawezi kuwekwa na ndugu zao, kati ya wengine.

- Ufuatiliaji wa watoto waliorejeshwa kwenye familia zao unapaswa kufanyika kwa kutumia njia mpya za uzuiaji wa maambukizi kutokana na vizuizi vilivyowekwa kwenye usafiri na mawasiliano ya kijamii.

- Maunganisho ya kifamilia na mawasiliano yanapaswa kuwezeshwa kwa mbali kwa watoto walio katika malezi ya familia za kuaminika na makao , ikiwa ni pamoja na kutafuta ushiriki wa walezi wakuu katika maamuzi muhimu juu ya mtoto. Kila juhudi zinahitajika kufanywa ili kuhakikisha njia za mawasiliano zinapatikana kwa watoto na walezi wa watoto wenye ulemavu.

**REJEA**

[16] Advice on the Use of Masks in the Context of COVID-19 (WHO)

## TUMIA TEKNOLOJIA KUWASILIANA NA KURATIBU KWA UFANISI



**Wafanyakazi wa huduma za jamii** wanapaswa kufikiria upya njia za kudhibiti kesi za COVID-19- Tathmini, utambuzi wa hatari, msaada na ufuatiliaji kupitia simu ya kawaida au anwani nyingine yoyote.

**Anzisha** taratibu za uchunguzi wa rufaa kupitia njia ya mtandaoni au ya simu, tathmini ya umuhimu wa uwekwaji watoto katika vituo vya malezi, idhini ya watoto kuwekwa kwenye vituo vya malezi na ufuatiliaji.

**Waunganishe wazazi / walezi na watoto wanaojulikana kuwa** katika hatari na watu wengine- Majukwaa ya mtandaoni, vikundi vya majadiliano vya WhatsApp na njia zingine za simu na njia za kawaida zinaweza kupunguza sana tatizo la watoto kutengwa.

**Rufaa** zinazojumuisha watoto wenye matatizo ya akili na msaada wa kisaikolojia pamoja na rasilimali za mtandaoni zinapaswa kupitiwa upya.

**Imarisha** uwezo wa huduma za simu na vituo vya msaada vya watoto, ili watoto, familia na vituo vya kutunzia watoto viweze kuripoti kesi yoyote ya unyanyasaji au kupuuz.

**Njia za hewa za uandikishaji wa watoto zinapaswa kutumika** (i.e., redio mtandaoni au kupitia televisheni,)  zikilenga hasa wanafamilia wajitolea wa utunzaji wa watoto ambao walipitishwa hapo zamani ambapo pengine hawajihusishi na huduma za malezi kwa sasa.

**Maunganisho na mawasiliano ya kifamilia** yafanyike kwa njia za mbali. Kila jitihada zinatakiwa kufanyika kuhakikisha njia za mawasiliano zinapatikana kwa watoto na walezi wenye ulemavu.

**Njia mpya** za kujishughulisha na masomo, shughuli za burudani, kuboresha afya na ukakamavu, kupata ujuzi wa maisha na malengo ya ufundi, na kupokea huduma wakati kukiwa na vizuizi na kufungwa kwa miji.

**Hakikisha** taratibu za usalama zinapitiwa upya ili kupunguza hatari zozote zitokanazo na kuongezeka kwa matumizi ya teknolojia.

*Picha Na: Brian McGowan,Unsplash*

Nyumbani
Utangulizi
Madhara
Njia
Malezi ya Familia
Malezi Mbadala
Mazingira ya Mtaani
Wanaondoka kwenye Malezi
Taarifa zaidi

- Wataalam wa ulinzi wa watoto wanapaswa kufanya kazi na viongozi wa jamii, wafanyakazi wa afya na wafanyakazi wa elimu kutambua familia zenye mazingira hatarishi kwa malezi ya mtoto. Kwa sasa, kigezo cha mazingira kuwa hatarishi ni pamoja na sifa ya mazingira ikiwa yanaweza kuwafanya walezi wa watoto au watoto kupata ugonjwa ikiwa eneo hilo lina virusi vya COVID-19; pia kusitishwa kwa huduma za malezi kwa sababu ya mlezi kukosa uwezo wa utunzaji kutokana na kukosa nyumba na makazi, huduma za jamii, au unyanyapaaji na ubaguzi.

- Katika mazingira ya hatari kubwa, wafanyakazi na mashirika yao wanapaswa kuhakikisha, inapowezekana, kuwa mawasiliano ya kawaida kwa njia ya simu au mtandao yanafanyika kila wakati (mf, mara tatu kwa wiki) na kwamba mipango ya msaada ya dharura inaandaliwa mapema kabla ya wakati[17]. Mipango inapaswa kuandaliwa kwa kumshirikisha mlezi na mtoto, wazazi na wanafamilia wengine. Mipango inapaswa pia kujadiliwa na (na kukubaliwa ku) mapema kwa walezi muhimu mbadala[18].

- Kwa familia zilizo hatarini zisizo na simu au mtandao, msimamizi wa mashauri akiwa na vifaa sahihi vya kijikinga wanapaswa kuendelea kutembelea familia kwa kuzingatia mwongozo wa afya na taratibu za umma zilizokubaliwa.

- Pale mtoto anapokuwa na mahitaji maalumu, ikiwa ni pamoja na changamoto za kimhemko na tabia, yuko katika hatari za kunyonywa/kudhulumiwa, au kuna shida fulani, kama kifo katika familia, au mlezi wa mtoto kupata maradhi, huduma ya rufaa ya mikutano ya kifamilia inaweza ikatolewa. Mamlaka za mtaa zinaanza kuitisha mikutano ya kikundi cha familia, kwa mfano kupitia WeChat, WhatsApp, Skype au Zoom, kukubaliana juu ya mipango ya mpito katika kipindi cha janga.

**MAREJELEO**

[17] Ethical Decision-Making in the Face of COVID-19 (IFSW)

[18] Guidelines for Virtual Monitoring of Children During COVID-19 (BCN)




*Picha Na: Save the Children*

Nyumbani
Utangulizi
Madhara
Njia
Malezi ya Familia
Malezi Mbadala
Mazingira ya Mtaani
Wanaondoka kwenye Malezi
Taarifa zaidi

# ULINZI WA WATOTO KATIKA MAZINGIRA YA MTAANI

Watoto walio mitaani hutegemea huduma zinazotolewa kupitia vituo vya muda mfupi vya huduma ili kukidhi mahitaji yao ya msingi. Watoto hawa mara nyingi huwa na hali mbaya ya kiafya na wanaweza kuwa hatarini zaidi kupata COVID-19[19]. Kwa kuongezea, watoto hawa wanaweza kujikuta katika hatari ya unyanyasaji wa kingono na ukatili ikiwa wanaishi peke yao mitaani, haswa katika hali ya sasa, ambapo watoto wengine / wakubwa ambao huwa wanaishi nao wanaweza kuwa wameondoka maeneno ya mijini. Wengi wa watoto hawa pia wanajitafutia riziki yao wenyewe, na inawezekana wakajikuta wanakosa kipato kutokana na hatua zilizowekwa za kukabiliana na janga hili na hivyo wanahitaji msaada zaidi ili waweze kuishi.

## Nini kifanyike kuwalinda watoto waishio mitaani

- Serikali na asasi za kiraia zinapaswa kuhakikisha kuwa vituo vya muda mfupi vya huduma na vituo vingine kama hivyo vinaandaliwa kama sehemu za huduma muhimu na vinakuwa na elimu ya kutosha juu ya maambukizi ya COVID-19, pamoja na huduma muhimu kama afya, usafi, ulinzi, elimu, na lishe.
- Polisi wanapaswa kuelekezwa ili kuhakikisha kuwa watoto waishio mitaani hawakamatwi kwa sababu ya kutojitenga, na badala yake, wanapaswa kusaidiwa ili wapate makazi au nyumba nyingine mbadala za kutosha, na kuunganishwa na huduma za afya pamoja na vituo vya ulinzi wa watoto kupitia vituo vya huduma kwa watoto[20].



*Picha Na: Boram Kim on Unsplash*

**MAREJELEO**

[19] Haki Za Wananchi Za Kinondoni Na Zaida Za Kiwangerezo
[20] Technical Note: COVID-19 and Children Deprived of their Liberty

## KUSAIDIA VIJANA WASIO KATIKA MALEZI NA WANAOISHI KWA KUJITEGEMEA

Vijana ambao wako kwenye kipindi cha mpito kutoka mfumo wa malezi mbadala (wanaoondokana na malezi) wanakabiliwa na hatari kubwa katika kipindi hiki cha COVID-19. Vijana wengine wanaweza kuwa katika harakati za kuondoka katika vituo vya malezi mbadala na kwenda kujitegemea katika kipindi sawia na mwanzo wa janga. Wanaweza kuwa miongoni mwa wale walioathiriwa zaidi na athari za muda mrefu kwani tayari wanakabiliwa na changamoto kubwa kupata elimu na fursa za kuishi sambamba na utengwaji na unyanyapaaji ulioenea.

### Nini kifanyike kuwasaidia vijana walioondokana na malezi mbadala na wale wanaojitegemea

- Wafanyakazi katika vituo vya malezi wanapaswa kuwasiliana na vijana au watoto wengi walioondoka kwenye vituo vya malezi mbadala na wanaoishi peke yao na kufanya uchunguzi wa awali ili kuangalia ustawi wao, kutathmini mahitaji yao ya msaada na kuwapa habari ya msingi juu ya kujikinga na COVID-19.
- Mashirika yanapaswa kuwapa kipaumbele vijana au watoto walioondoka kwenye vituo vya malezi ambao hawajapata malazi na njia bora za maisha, huku wakiwapa msaada wa dharura unaowalenga wao. Wafanyakazi wa malezi wanapaswa kufanya kazi na mashirika mama ya kwao ili kuhakikisha kuwa mipangilio kama vile vocha inapatikana kwa vijana ili waweze kununua vifaa muhimu kwa ambao watakabiliwa na ukosefu wa fedha kwaajili ya mahitaji yao ya kila siku.
- Mashirika yanapaswa kuwezesha upatikanaji wa huduma ya afya ya akili na msaada wa kisaikolojia, ikiwa ni pamoja na huduma za msaada wa afya ya akili zitakazokuwa zikitolewa kwa njia ya mtandao na kwa kuwezesha mawasiliano ya mara kwa mara na walezi kupitia huduma za simu au mtandao.
- Wafanyikazi wa malezi wanapaswa kusaidia vijana wanaoishi kwa kujitegemea, hasa katika makazi ya pamoja / kikundi, kukubaliana kwa pamoja juu ya sheria fulani za msingi ili kuhakikisha utekelezwaji mzuri wa kukaa mbalimbali, kujitenga na mahitaji ya karantini.
- wHuduma za utetezi na vikundi vya misaada huchukua jukumu muhimu kutoa msaada wa vitendo, mwongozo na ushauri. Kuongeza ufadhili kwa mashirika haya ili kuwawezesha kukuza huduma za msaada wao wa simu na mtandaoni na kufanya waongeze upeo wa kazi zao. Kwa mfano, kupitia vikundi vya WhatsApp vilivyorekebishwa, ambapo vijana wanawezakusaidiwa kuanzisha “mifumo ya urafiki” na wenzao ili kuwasiliana, kuangalia ustawi wa kila mmoja, afya, na kutoa msaada wakati unahitajika.

# TAARIFA ZAIDI

Better Care Network (BCN): Resource Center on COVID-19 and Children's Care
https://bettercarenetwork.org/library/particular-threats-to-childrens-care-and-protection/resource-center-on-covid-19-and-childrens-care

The Alliance for Child Protection in Humanitarian Action:
https://alliancecpha.org/en/COVD19

UNICEF:
https://www.unicef.org/coronavirus/covid-19

International Disability Alliance (IDA):
http://www.internationaldisabilityalliance.org/content/covid-19-and-disability-movement

Early Childhood Development Action Network (ECDAN):
https://www.ecdan.org/

COVID-19 Parenting:
https://www.covid19parenting.com/

Inter-agency Network for Education in Emergencies (INEE):
https://inee.org/collections/coronavirus-covid-19

Global Social Service Worker Alliance (GSSWA):
http://socialserviceworkforce.org/resources/blog/social-service-workers-mitigating-impact-covid-19

International Organization for Migration (IOM):
https://www.iom.int/covid19

## SHUKURANI

**Mashirika na watu binafsi wafuatao wamechangia katika uandaaji wa dokezo hili la kiufundi.**

The Alliance for Child Protection in Humanitarian Action
Better Care Network
Catholic Relief Services
The Centre for Excellence for Children's Care and Protection (CELCIS)
Changing the Way We Care
CRIN
Family for Every Child
Faith to Action Initiative
Hope and Homes for Children
International Disability Alliance
International Organization on Migration (IOM)
International Rescue Committee (IRC)
International Social Service
LUMOS
Maestral International
The Martin James Foundation
Office of the Special Representative of the Secretary-General on Violence Against Children
Plan International
RELAF
Save the Children
SOS Children's Villages International
UNHCR
UNICEF
World Vision
John Williamson, Children in Adversity, USAID
Joan Lombardi (Early Opportunities)
Shukrani kwa Shirika la Afya Duniani (WHO)  kwa kupitia rasimu ya kazi hii

**Dokezo hili la kiufundi limethibitishwa na mashirika yafuatayo**

Design: www.prinsdesign.co.za   Cover photo by Volodymyr Hryshchen, Unsplash